# JARIDA *la*

## *Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA)*

JARIDA MAALUMU | TOLEO LA KWANZA | JANUARI - MACHI 2026









**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA AHADI ZA SIKU 100 ZA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN** UK.15 $ 16




temesa tanzania

# YALIYOMO


03 Waziri Mkuu apongeza mchango wa TEMESA katika kukuza mawasiliano

04 Waziri Mkuu aagiza malipo ya haraka kukamilisha vivuko Kigamboni

05 Waziri Ulega awataka wakandarasi kuongeza kasi ya ujenzi wa kivuko kipya Mafia-Nyamisati

06 Serikali yatoa trilioni 1.319 kuimarisha miundombinu, ulega aeleza mafanikio Sekta ya Ujenzi

07 Mkuu wa Mkoa Mwanza aipongeza serikali kwa uwekezaji mkubwa Ziwa Victoria

09 Vivuko vipya vyakamilika, kufungua fursaza kiuchumi kwa wakazi Ukerewe

10 Temesa yashiriki maonesho mafanikio siku100 za Rais Samia na utatuzi wa kero za wananchi

11 Muongozo wa matumizi ya "WALLET"

13 Matukio katika Picha

15 Taarifa ya utekelezaji wa ahadi za siku 100 za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan




# BODI YA UHARIRI


**MWENYEKITI**
MOSES RAJAB MABAMBA
*KAIMU MTENDAJI MKUU*

**MHARIRI MKUU**
MARTHA JOACHIM
*MENEJA MASOKO NA UHUSIANO KWA UMMA*

**WAJUMBE**
NELSON RWECHUNGURA
*MENEJA RASILIMALI WATU*

STANLEY MULIBO
*MENEJA UTAWALA*

NOEL MAROBE
*KAIMU MKAGUZI WA NDANI MKUU*

CHRISTIAN MAKAWA
*MHASIBU MKUU*

JACKSON MATANDU
*MENEJA MIPANGO, TAFITI NA UBUNIFU*

**WAANDISHI**
SAMSON MRUTU
ALFRED MGWENO
SALAMA NKONYA
JOVIN MBEGHA

**MSANIFU KURASA**
NEEMA MACHA




# NENO LA UTANGULIZI



Katika ulimwengu wa leo unaoendeshwa na kasi kubwa ya maendeleo ya teknolojia pamoja na kuongezeka kwa mahitaji ya huduma bora, Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) umeendelea kujidhihirisha kama nguzo muhimu katika kuhakikisha miundombinu ya Serikali katika matengenezo na taasisi yake inakuwa salama, imara na yenye kuaminika. Nafasi yake imeendelea kuwa ya msingi katika kusaidia utekelezaji wa majukumu ya Serikali kwa ufanisi na uhakika.

Kupitia uwekezaji endelevu katika rasilimali watu, ununuzi wa vifaa vya kisasa, pamoja na matumizi ya mifumo ya kidijitali, TEMESA imefanikiwa kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma zake kuanzia matengenezo ya magari ya Serikali, usimamizi wa mitambo ya umeme, hadi utoaji wa ushauri wa kihandisi, taasisi hii imeendelea kuwa mhimili muhimu katika kuendeleza maendeleo ya Taifa.

Mafanikio haya hayawezi kutenganishwa na mchango mkubwa wa wafanyakazi wake, ambao nidhamu, weledi na uzalendo wao umeendelea kuwa chachu ya mafanikio. Hivyo, ni muhimu kuendeleza utamaduni wa uwajibikaji, ubunifu na kujifunza endelevu ili kukabiliana vyema na changamoto zinazoletwa na mabadiliko ya teknolojia na matarajio ya wateja.

TEMESA inaendelea kusisitiza misingi ya uadilifu na kupambana na rushwa, kwa kuzingatia kuwa uwazi na maadili bora ni nguzo muhimu katika kujenga imani kwa umma na wadau wake.

Katika kuhakikisha ustawi wa wafanyakazi, juhudi zimekuwa zikifanyika kuhamasisha afya bora, ikiwa ni pamoja na kujikinga na magonjwa ya kuambukiza na yasiyoambukiza. Afya ya mfanyakazi ni mtaji mkubwa wa taasisi yoyote yenye mafanikio.

Tunapoendelea mbele, ni wajibu wetu sote kushirikiana katika kuifanya TEMESA kuwa kitovu cha ubora na ubunifu, tukihakikisha huduma zetu zinakidhi viwango vya kimataifa na kuchangia kikamilifu katika maendeleo endelevu ya Taifa letu.

***"Huduma bora kwa Fursa za Maendeleo"***

**Wakili. Moses Mabamba**
**Kaimu Mtendaji Mkuu.**
**TEMESA.**




# WAZIRI MKUU APONGEZA MCHANGO WA TEMESA KATIKA KUKUZA MAWASILIANO YA KIMKAKATI

*Na Martha Joachim, TEMESA*

Tarehe 25 Machi, 2026, Wakala wa Ufundi na Umeme TEMESA ulishiriki Mkutano wa 110 wa mafunzo kwa watayarishaji wa vipindi vya elimu kwa Umma. Mkutano huo wa mafunzo ulifanyika katika ukumbi wa mikutano wa Ubuntu jengo la Posta la PAPU lililoko jijini Arusha na kufunguliwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba.

Waziri Mkuu akihutubia wakati wa mkutano huo, ameipongeza TEMESA kwa mchango wake katika kuimarisha mawasiliano ya kimkakati yanayofanywa na Maafisa Habari wa Taasisi mbalimbali za Umma.

Waziri Mkuu Dkt. Mwigulu amesisitiza umuhimu wa taasisi za Umma kushirikiana na vyombo vya habari kufanya mawasiliano ya kimkakati katika kuongeza uelewa kwa jamii kuhusu utekelezaji wa mipango ya maendeleo inayotekelezwa na Serikali.

Kwa upande wake, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Christian Makonda ameeleza kuwa Wizara itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali, hususani wadau wa kutoa Elimu kwa Umma na vyombo vya habari ili kuhakikisha wananchi wanapata taarifa sahihi kuhusu miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan.

TEMESA ni moja ya taasisi za Umma zilizoshiriki na kudhamini mkutano huo uliowakutanisha Maafisa Habari kutoka taasisi mbalimbali za Umma pamoja na wadau wa mawasiliano. Mkutano huo ulianza tarehe 23 Machi, na kuhitimishwa tarehe 27 Machi, 2026.

# WAZIRI MKUU AAGIZA MALIPO YA HARAKA KUKAMILISHA VIVUKO KIGAMBONI

*Na Samson Mrutu, TEMESA*

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba, ameielekeza Wizara ya Ujenzi kuwasiliana kwa haraka na Wizara ya Fedha ili kuhakikisha inakamilisha malipo ya ujenzi wa vivuko vilivyopo kwenye hatua za ukarabati, kwa lengo la kuviwezesha kurejea kutoa huduma kwa wananchi wa Kigamboni, jijini Dar es Salaam.

Waziri Mkuu Mhe. Dkt. Nchemba ametoa agizo hilo alipofanya ziara ya kushtukiza kukagua hali ya utoaji wa huduma ya vivuko katika eneo la Magogoni. Waziri Mkuu alisema kuwa kukamilika kwa malipo hayo kutaharakisha kurejea kwa vivuko hivyo kazini, hatua itakayosaidia kupunguza kero ya usafiri kwa wakazi wa Kigamboni na maeneo ya jirani.

“Mhe. Waziri, naomba muwasiliane haraka na Wizara ya Fedha ili fedha zinazohitajika ziweze kutolewa kwa wakati, vivuko hivi vikamilike na virejee kutoa huduma hapa Magogoni,” amesema Waziri Mkuu.

Aidha, Dkt. Nchemba amesisitiza kuwa malipo hayo yafanyike ndani ya kipindi cha mwezi mmoja, huku akiwataka viongozi wa sekta husika kusimamia kwa karibu utekelezaji wa ukarabati huo ili kuhakikisha kazi inakamilika kwa wakati na kwa viwango vinavyotakiwa.

“Fedha zitakapotolewa, hakikisheni kuwa wakandarasi wanakamilisha kazi kwa haraka. Lengo letu ni kuona vivuko vinarejea mapema kutoa huduma, na hivyo kuondoa changamoto za usafiri zinazowakabili wananchi wetu,” amesisitiza.

Ziara hiyo imelenga kuonyesha dhamira ya Serikali ya kuboresha huduma za usafiri wa maji, hasa katika maeneo yenye uhitaji mkubwa kama Kigamboni, na kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora, salama na kwa wakati.



# WAZIRI ULEGA AWATAKA WAKANDARASI KUONGEZA KASI YA UJENZI WA KIVUKO KIPYA MAFIA–NYAMISATI

*Na Jovin Mbegha, TEMESA*

Waziri wa Ujenzi, Mhe. Abdallah Ulega, ametembelea eneo la kata ya Kimbiji, wilayani Kigamboni kwa ajili ya kukagua maendeleo ya mradi wa ujenzi wa kivuko kipya kitakachokwenda kutoa huduma kati ya Mafia na Nyamisati.

Lengo la ziara ya Waziri wa Ujenzi lilikuwa ni kujionea kwa macho hatua zilizofikiwa na mkandarasi katika ujenzi wa kivuko hicho kipya ambacho kinasubiriwa kwa hamu na wakazi wa maeneo hayo ambao kwa sasa wanategemea kivuko kimoja tu cha MV. KILINDONI.

Akiwa ziarani, Waziri Ulega amemuagiza mkandarasi anayetekeleza mradi wa ujenzi wa kivuko hicho kipya cha Mafia–Nyamisati kuongeza kasi ya utekelezaji wa mradi huo na kuhakikisha anamaliza kazi hiyo kwa viwango vya juu na ndani ya muda uliopangwa.

Waziri Ulega amemsisitizia mkandarasi anayesimamia ujenzi wa kivuko hicho Dar es Salaam Maritime Group (DMG) afanye kazi kwa uharaka na weledi kwa kuwa mradi huo ni wa kimkakati kwa ustawi wa wananchi wa Mafia Mkoani Pwani, hivyo ni muhimu kazi ifanyike kwa kasi na weledi



"Nasisitiza mkandarasi afanye kazi usiku na mchana. Ongezeni vijana zaidi kwenye kazi hizi, kwani tuna vijana wengi wa Kitanzania wanaotafuta fursa za ajira. Lengo ni kuhakikisha mradi huu unakamilika kwa wakati na kwa ubora unaostahili," alisema Waziri Ulega.

Aidha, ameelekeza kuwa watumishi wote waliopata nafasi ya kushiriki katika mradi huu wapewe vyeti vya kutambua ushiriki wao, ili kuwajengea uwezo na kuwaandaa kushiriki katika miradi mingine ya kitaifa siku zijazo.

Akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa mradi huo, Kaimu Mtendaji Mkuu wa TEMESA, Wakili. Moses Rajab Mabamba, amesema kuwa kutokana na mahitaji makubwa ya wananchi, Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi imetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa kivuko hicho kipya.

Wakili. Mabamba amebainisha kuwa mradi umefikia asilimia 57 ya utekelezaji na kivuko hicho kitakapokamilika kitakuwa suluhisho la muda mrefu kwa changamoto za usafiri kati ya Mafia na Nyamisati, na pia kuchochea shughuli za kiuchumi katika maeneo hayo.

Kwa upande wake Mbunge wa Kigamboni, Mhe. Sanga Nyakisa, ameiomba Wizara kutatua changamoto za vivuko vya MV. KIGAMBONI na MV. MAGOGONI, akisema vimekuwa vikiwasababishia wananchi wa Kigamboni kero kubwa ya usafiri.

# SERIKALI YATOA TRILIONI 1.319 KUIMARISHA MIUNDOMBINU, ULEGA AELEZA MAFANIKIO SEKTA YA UJENZI



*Na Mwandishi, Wizarani*

Mnamo Tarehe 23 Machi, 2026, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu imekutana na Waziri wa Ujenzi pamoja na Watendaji wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo.

Waziri wa Ujenzi, Mhe. Abdallah Ulega, ameieleza Kamati hiyo ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuwa Serikali imeendelea kupiga hatua katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo hadi kufikia Machi 2026, jumla ya shilingi trilioni 1.319 tayari zilikwisha tolewa kwa ajili ya miradi iliyoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2025/2026.

Akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa mpango na bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026 pamoja na makadirio ya mwaka 2026/2027 kwa fungu 98 la Wizara ya Ujenzi Machi 23, 2026 Mkoani Dodoma, Ulega ameeleza fedha hizo ni sawa na asilimia 72.80 ya bajeti iliyoidhinishwa na kubainisha mafanikio yaliyopatikana hadi kufikia Machi, 2026.

Waziri Ulega akiizungumzia Sekta ya vivuko, ameeleza kuwa Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) umekamilisha maegesho ya kivuko ya Ijinga Kahangala, Bwiro Bukondo pamoja na Kisorya–Rugezi–Bukimwi, sambamba na kukamilisha ujenzi wa kivuko MV. UKEREWE kitakachotoa huduma kati ya Kisorya Wilayani Bunda Mkoani Mara na Rugezi Wilayani Ukerewe Mkoani Mwanza, vile vile Mhe. Ulega alisema kuwa Serikali imekamilisha ujenzi wa kivuko MV. BUKONDO kitakachotoa huduma kati ya Bwiro na Bukondo Wilayani Ukerewe Mkoani Mwanza pamoja na kukamilisha ukarabati wa boti ya dharura ya MV. TANGAZO inayotoa huduma Mkoani Mtwara.

Ulega amesisitiza kuwa katika mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara ya Ujenzi itahakikisha inatekeleza kwa vitendo maono na dira ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuwaletea Watanzania maendeleo endelevu kupitia miundombinu bora, salama na yenye tija.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mhe. Selemani Kakoso, ameipongeza Wizara hiyo kwa juhudi zake katika kusimamia na kutekeleza miradi ya kimkakati, hususan ujenzi wa vivuko, barabara na madaraja unaorahisisha usafiri na usafirishaji wa mizigo na abiria nchini.

# MKUU WA MKOA MWANZA AIPONGEZA SERIKALI KWA UWEKEZAJI MKUBWA ZIWA VICTORIA

*Na Alfred Mgweno, TEMESA*

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Mhe. Said Mtanda ameipongeza Serikali ya Awamu ya Sita kwa uwekezaji mkubwa inaoendelea kuufanya katika Ziwa Victoria ikiwemo kuboresha huduma za usafiri wa vivuko. Mhe. Mtanda ameyasema hayo Tarehe 16 Septemba, 2025 wakati alipokuwa akishuhudia kivuko MV. BUKONDO kikishushwa kwenye maji kwa ajili ya kuanza kufanyiwa majaribio baada ya ujenzi wake kukamilika.

Mkuu wa Mkoa amesema kuwa mradi huo wa ujenzi wa kivuko MV. BUKONDO ni mradi mkubwa na unaenda kuepusha ajali ambazo zimekuwa zikitokea mara kwa mara katika visiwa hivyo kutokana na wananchi hao kukosa huduma ya uhakika ya usafiri hali ambayo inawalazimu kutumia mitumbwi midogo na boti za mbao ambazo sio salama kwa ubebaji wa mizigo na abiria wanaosafiri masafa marefu.

Mhe. Mtanda pia ametumia fursa hiyo kuishukuru Serikali kwa kutekeleza miradi ya usafiri wa maji kwa wakazi wa Mkoa wa Mwanza, ‘’kwahiyo kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Mwanza, nichukue fursa hii kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri aliyoifanya na kwa uwekezaji mkubwa alioufanya ndani ya Ziwa Victoria,’’ alisema Mtanda na kuendelea kumpongeza Mhe. Abdallah Ulega, Mtendaji Mkuu wa TEMESA pamoja na mkandarasi Songoro Marine ambaye amejenga kivuko hicho na vingine.

Mkurugenzi wa Uendeshaji na Ujenzi wa Vivuko TEMESA mhandisi Lukombe King’ombe akizungumza wakati wa tukio hilo amesema kivuko cha MV. BUKONDO kina uwezo wa kubeba tani 100, abiria 200 pamoja na magari madogo 10. Mhandisi King’ombe ameongeza kuwa baada ya zoezi la kushusha kivuko MV. BUKONDO, kivuko kitakachofuatia kushushwa kwenye maji ni MV. UKEREWE. Alisema kuwa kivuko cha MV. UKEREWE ambacho kitakwenda kutoa huduma kati ya Kisorya Wilayani Bunda Mkoani Mara na Rugezi Wilayani Ukerewe Mkoani Mwanza, kina uwezo wa kubeba tani 170, abria 800 pamoja na magari 22 na kuongeza kuwa vivuko vyote vimejengwa kwa kuzingatia sheria za kimataifa za ujenzi wa vyombo vya maji.



“Vivuko hivi vyote vinavyojengwa hapa vimezingatia ubora wa vifaa vyote ambavyo vinahitajika kwenye vyombo vya majini, vyombo hivi ni vya kisasa vina vifaa vyote vya kuongozea meli vya kisasa, kwahiyo tunatarajia wananchi katika maeneo husika watapata huduma wanayoitarajia kutokana na ujio wa vivuko hivi.’’ Alisema Mhandisi King’ombe.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Songoro Marine, Major Songoro akizungumza na waandishi wa habari amesema kuwa tukio hilo ni tukio kubwa na la furaha kwa kampuni hiyo kuweza kumaliza ujenzi wa kivuko hicho pamoja na vivuko vingine na ni hatua kubwa ambayo inapaswa kupongezwa.

Ameipongeza Serikali, Wizara ya Ujenzi pamoja na TEMESA kwa kuweza kufanikisha ukamilishaji

wa mradi huo huku akiwaasa wakazi wa Bukondo na Bwiro kuendelea kutoa shukrani kwa Serikali.

“Serikali kwa kweli inapiga kazi kubwa sana, kwahiyo wakazi wa Bukondo wawe na imani na Serikali yao ukiangalia hiki chombo pesa nyingi sana imeingia kujenga hiki chombo”, alisema Songoro na kuendelea kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kujenga Taifa na kuboresha miundombinu ya usafiri wa maji.



# KAMATI YA MIUNDOMBINU YAPITISHA RANDAMA YA BAJETI WIZARA YA UJENZI 2026/2027.



*Na Mwandishi , Wizarani*

Tarehe 24 Machi, 2026 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu imekutana na Waziri wa Ujenzi pamoja na Watendaji wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo mjini Dodoma.

Kamati hiyo imepitisha Randama ya Mpango na Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2026/2027 ya Wizara ya Ujenzi hatua iliyotajwa kuwa muhimu katika kuendeleza kasi ya uboreshaji wa miundombinu nchini.

Mhe. Selemani Kakoso ni Mwenyekiti wa Kamati hiyo, akizungumza katika kikao hicho jijini Dodoma, Mhe. Selemani Kakoso, amesema uamuzi huo unaenda sambamba na dhamira ya kuhakikisha miundombinu ya kisasa inaendelea kujengwa na kuboreshwa ili kuchochea maendeleo ya kiuchumi kwa wananchi na Taifa kwa ujumla.

Kwa upande wake, Waziri wa Ujenzi, Mhe. Abdallah Ulega ameishukuru Kamati hiyo kwa kuidhinisha randama hiyo na kuahidi kuwa Wizara itaendelea kusimamia kwa karibu utekelezaji wa miradi ya kimkakati ili kuhakikisha inakamilika kwa viwango bora na kuleta manufaa kwa wananchi.

# VIVUKO VIPYA VYAKAMILIKA, KUFUNGUA FURSA ZA KIUCHUMI KWA WAKAZI UKEREWE




Na Salama Nkonya, TEMESA

Serikali kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) imekamilisha rasmi ujenzi wa vivuko vipya viwili kati ya vitano vinavyojengwa na kampuni ya Songoro Marine Transport Boatyard iliyoko mjini Mwanza.

Vivuko hivyo viwili ni MV. UKEREWE kinachokwenda kutoa huduma kati ya Kisorya Wilayani Bunda Mkoani Mara na Rugezi Nansio Wilayani Ukerewe Mkoani Mwanza pamoja na kivuko MV. BUKONDO kinachokwenda kutoa huduma kati ya Bwiro na Bukondo Nansio Ukerewe Mkoani Mwanza.

Mhandisi Lukombe King'ombe ni Mkurugenzi wa Uendeshaji na Ujenzi wa vivuko TEMESA ambaye amefika Mkoani Mwanza kwa ajili ya kukagua vivuko hivyo mara baada ya ujenzi wake kukamilika.

Akizungumza mara baada ya kukagua vivuko hivyo viwili na kuvifanyia majaribio (Sea/ Lake Trial) katika Ziwa Victoria ambako vivuko hivyo vilitembea kwa zaidi ya saa tatu, Mhandisi King'ombe amesema kuwa kukamilika rasmi kwa ujenzi wa vivuko hivyo viwili kutasababisha kufunguka kwa fursa za kiuchumi na huduma za kijamii kwa wanachi wanaoishi maeneo hayo kwani kwa muda mrefu wamekuwa wakitumia mitumbwi na boti ndogo za mbao kwa ajili ya kusafiri kutoka eneo moja la kisiwa kwenda eneo jingine hali iliyokuwa ikiwahatarishia usalama wa maisha na mali zao.

Mhandisi King'ombe amesema kuwa adhma kubwa ya timu iliyokwenda kukagua vivuko hivyo viwili kutoka Chuo cha Bahari Dar es Salaam DMI na Wizara ya Ujenzi ni kuhakikisha vivuko hivyo viko tayari kwa kuanza kazi ambako walikagua injini za vivuko hivyo vyote, mitambo na mifumo ya uendeshaji wa vivuko hivyo, vifaa vya uokozi na usalama yakiwemo maboya ya uokozi, boti za dharura za uokozi, mifumo ya kutambua mioto na mifumo ya kuzimia mioto.

"Adhma kubwa ya timu hii kuja kukagua vivuko hivi ni kwa ajili ya maandalizi sasa ya kupekeka vivuko hivi katika maeneo ambavyo vitahudumu, kwahiyo sisi kama timu tumemuwakilisha Mtendaji Mkuu wa TEMESA kwa ajili ya ukaguzi wa mwisho baada ya vivuko hivi kukidhi vigezo vya ubora kwa maana ya mifumo ya uendeshaji pamoja na vifaa kwa ajili ya usalama wa abiria wanapokuwa ndani ya vivuko."

Mhandisi King'ombe ameongeza kuwa vivuko hivyo pia tayari vilipitiwa na kukaguliwa na wataalamu kutoka Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) na tayari walishatoa vyeti vya ubora ili kuweza kuruhusu vivuko hivyo kwenda kuhudumu katika maeneo ambayo vinapaswa kutumika.

Aidha Mhandisi King'ombe ameongeza kuwa walifanya majaribio (Sea/Lake Trial) ya vivuko hivyo na wakajiridhisha kwamba vifaa vyote vya vivuko hivyo vinafanya kazi ambayo ni tayari kwa ajili ya kwenda

kuhudumu.

Halikadhalika, timu hiyo ilipata pia wasaa wa kutembelea maegesho ya vivuko hivyo ambayo tayari yamekamilika kwa asilimia kubwa. Mhandisi King’ombe amesema kuwa Serikali tayari imekamilisha ujenzi wa mindombinu ya maegesho ya vivuko hivyo ambako vivuko hivyo vitakuwa vinapaki kwa ajili ya kupakia na kushusha abiria na mizigo.

“Timu hii pia ilitembelea kwenye maeneo hayo ya maegesho ili kujiridhisha kuwaleta viongozi kwa ajili ya uzinduzi na kupekeka hii huduma kwa wananchi na kufungua fursa za kiuchumi, ni matarajio yetu kwamba vivuko hivi vinakwenda kufungua fursa za kiuchumi kwa wananchi na kuwarahisishia majukumu yao kwasababu katika eneo lile la Bwiro Bukondo wote mnafahamu wananchi wanatumia mitumbwi kwahiyo kwa sasa mitumbwi basi tunawapelekea vivuko vikafungue fursa kwa wananchi wa maeneo haya.” Alisistiza Mhandisi King’ombe.

Kivuko cha MV. UKEREWE kina uwezo wa kubeba tani 170, abiria 800 na magari 22 wakati kivuko MV. BUKONDO kina uwezo wa kubeba tani 100, abiria 200 na magari 10. Vivuko hivyo viwili vimegharimu shilingi Bilioni 11 mpaka kukamilika ujenzi wake na fedha zote zimetolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

# TEMESA YASHIRIKI MAONESHO MAFANIKIO SIKU 100 ZA RAIS SAMIA NA UTATUZI WA KERO ZA WANANCHI

*Na Jovin Mbegha, TEMESA*




Mnamo Tarehe 4 mpaka 6 mwezi Machi, 2026, Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) ulishiriki maonesho ya mafanikio ya siku 100 za uongozi wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Maonesho hayo yalikuwa na lengo la kuhakikisha Taasisi za Umma na binafsi zinashiriki katika kutatua kero zinazowakumba wananchi kwenye kupatiwa huduma za kila siku za kijamii katika ofisi husika.

Katika maonesho hayo yaliyochukua siku tatu, TEMESA ilishiriki kwa kuwa na banda kwa ajili ya kusikiliza kero za wananchi lakini pia kuwaelezea namna TEMESA uinavyotekeleza majukumu yake.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Rosemary Senyamule amepata wasaa wa kutembelea banda la TEMESA ambapo Kaimu Meneja Masoko na Uhusiano Bi. Martha Joachim ameeleza mafanikio ambayo TEMESA imeyapata katika utoaji wa huduma kwa wananchi, maboresho makubwa yanayoendelea kufanyika katika Wakala pamoja na kutoa elimu kuhusu majukumu ya Wakala huo.

Bi. Martha ameeleza kuwa miongoni mwa mafanikio ambayo TEMESA imeyapata ni pamoja na matumizi ya Mfumo wa Usimamizi wa Kazi za Matengenezo (MUM) unaosaidia kurahisisha ufuatiliaji wa shughuli za matengenezo kwa urahisi zaidi.

Bi Martha ameongeza kuwa mfumo huo umeongeza uwazi, ufanisi na kasi katika utoaji wa huduma za matengenezo na kusaidia taasisi za Serikali kupata huduma bora

zinazopelekea kuwahudumia wananchi kwa ufanisi.

TEMESA inaendelea kuboresha utendaji kazi wake hasa katika huduma za matengenezo ya magari ya Serikali, usimamizi wa vivuko pamoja na miundombinu ya umeme katika taasisi mbalimbali za Umma.




# MUONGOZO WA MATUMIZI YA "WALLET"

## WATEJA KUWEKA FEDHA KWENYE WALLET

### Usajili wa Taasisi

Ili kutumia "Wallet", taasisi inapaswa kusajiliwa kwenye mfumo wa MUM. Usajili utahusisha majina ya maafisa wasiopungua watatu:
**i.** Mtumishi kutoka idara tumizi,
**ii.** Mtumishi kutoka idara ya uhasibu, na
**iii.** Mkuu wa Taasisi.

### Kufungua Akaunti ya Wallet

Baada ya usajili kukamilika, taasisi itafungua akaunti ya "Wallet" kupitia Sub Menu ya Wallet na kufuata maelekezo yaliyopo.

### Kuweka Fedha

Taasisi inapaswa kufungua Sub Menu ya My Wallet ili kuomba kuweka fedha. Baada ya taratibu zote za approvals kukamilika, taasisi itapokea Control Number ya malipo yenye kiasi kilichoombwa. Baada ya kufanya malipo kupitia benki au mitandao ya malipo, salio la Wallet litasasishwa moja kwa moja kwenye mfumo wa MUM.

## JINSI TAASISI ZITAKAVYOFANYA MATUMIZI YA WALLET

### Malipo kwa Huduma za TEMESA

Fedha zilizopo kwenye Wallet zitatumika kulipia huduma zote za TEMESA zinazopatikana kupitia mfumo wa MUM na pia katika vituo vyote vya uzalishaji vya Wakala.

Uchaguzi wa Njia ya Malipo Pindi taasisi itakaporidhia gharama zilizowasilishwa kupitia MUM, itachagua njia ya malipo kati ya: "Wallet" Kupatiwa Control Number ya huduma iliyoombwa.

### Muamala Kupitia Wallet

Iwapo taasisi itachagua Wallet, gharama husika zitapunguzwa kwenye salio la Wallet na kuelekezwa kwenye akaunti ya kituo kilichotoa makadirio ya kazi husika.

Baada ya muamala kukamilika, mteja atapokea taarifa zifuatazo:
**i.** Kituo cha TEMESA kitakachotoa huduma,
**ii.** Namba ya matengenezo,
**iii.** Namba ya muamala wa Wallet (Wallet Transaction Number),
**iv.** Tarehe ya muamala,
**v.** Aina ya huduma, na
**vi.** Kiasi kilichotumika.

## KUPATA TAARIFA ZA MATUMIZI YA WALLET

### Upatikanaji wa Historia ya Matumizi

Mteja au taasisi inaweza kupata taarifa za matumizi ya Wallet moja kwa moja kupitia mfumo wa MUM kwenye Sub Menu ya My Wallet History.

Aina za Taarifa Zinazopatikana

**i.** Kiasi kilichowekwa,
**ii.** Kiasi kilichotumika,
**iii.** Kazi zilizofanyika,
**iv.** Kituo kilichotoa huduma,
**v.** Tarehe ya miamala,
**vi.** Salio lililopo, na
**vii.** Historia ya miamala yote iliyofanyika.

# TEMESA NA MAADHIMISHO YA SIKU YA WANAWAKE DUNIANI MACHI 2026






# TEMESA NA MAADHIMISHO YA SIKU YA WANAWAKE DUNIANI MACHI 2026





# TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA AHADI ZA SIKU 100 ZA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN

*Na Alfred Mgweno, TEMESA*




Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) unatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia malengo na mikakati ya kitaifa na kimataifa ambayo yameainishwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, Tanzania Development Vision 2050, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2025, Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2025/26–2029/30), Mpango kazi wa Wizara ya Ujenzi, na Malengo ya Maendeleo Endelevu 2015–2030 (SDGs).

Aidha, katika kutekeleza majukumu yake, TEMESA umeendelea kuboresha utoaji wa huduma bora na stahiki kwa wananchi katika sekta za ufundi wa magari, umeme na elektroniki na huduma ya usafirishaji kwa njia ya maji kwa kutumia vivuko vya Serikali.

Mnamo tarehe 30 Oktoba 2025, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, alitoa ahadi kwa Watanzania kwamba ndani ya siku 100 Serikali yake itakuwa imetekeleza kikamilifu ahadi muhimu alizozitoa kwa wananchi.

Hadi sasa, utekelezaji wa ahadi hizo kwa upande wa Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) unaendelea kuonyesha mafanikio makubwa na ya kihistoria. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:

Katika siku 100 za uongozi wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Serikali kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) imefanikiwa kutoa fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa vivuko vipya viwili, kivuko cha MV. UKEREWE pamoja na kivuko cha MV. BUKONDO ambavyo vinakwenda kurahisisha utoaji wa huduma katika maeneo ambayo yamepelekwa kwa ajili ya kuwahudumia wananchi.

Kivuko MV. BUKONDO kinakwendakutoa huduma kati ya Bwiro na Bukondo Wilayani Ukerewe Mkoani Mwanza eneo ambalo halijawahi kuwa na kivuko hapo awali hivyo kupelekwa kwa kivuko hicho kunakwenda kurahisisha shughuli za kiuchumi na kijamii kwa wananchi wa maeneo hayo.

Kivuko MV. UKEREWE kinakwenda kutoa huduma kati ya Kisorya Wilaya ya Bunda Mkoa wa Mara na Rugezi Wilaya ya Ukerewe Mkoa wa Mwanza.

Katika siku 100 za uongozi wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) imeweza kutekeleza ukarabati wa vivuko MV. KAZI, MV. MAGOGONI na MV. KIGAMBONI.

Katika siku 100 za uongozi wake Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) imefanikiwa kukarabati kivuko MV. KAZI kinachotoa huduma kati ya Magogoni na Kigamboni

jijini Dar es Salaam ili kuongeza huduma ya usafiri kwa wananchi wa maeneo hsyo bila usumbufu.

Serikali pia imetoa fedha kwa ajili ya kukamilisha ukarabati wa kivuko MV. MAGOGONI ambacho kinafanyiwa ukarabati huko Mombasa nchini Kenya na ukarabati wake umefikia asilimia 81.3.

Serikali pia ndani ya siku 100 za uongozi wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imetoa fedha kwa ajili ya kukamilisha ukarabati wa Kivuko MV. KIGAMBONI ambacho kinafanyiwa ukarabati katika Yadi ya Songoro iliyoko Kigamboni jijini Dar es Salaam. Kivuko hicho pia kinatarajiwa kurejea kutoa huduma mwezi Novemba, 2026 mara baada ya ukarabati wake kukamilika.

Vivuko hivyo viwili vitakapokamilika na kurejea, vitarahisisha utoaji wa huduma katika eneo hilo kwa kiasi kikubwa.

Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA), kupitia Wizara ya Ujenzi umefanikiwa kuboresha na kuunda muundo mpya wa TEMESA wenye lengo la kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi na kuweka mazingira rafiki ya watumishi katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku.

Katika siku 100 za uongozi wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) imefanikiwa kuondoa rasmi uzalishaji wa madeni kutoka katika Wizara na Taasisi za Umma ambapo Wakala kwa sasa unatoa huduma kupitia mfumo wa malipo ya kabla (Pre-Paid).

Hatua hii imepunguza kwa kiasi kikubwa mzigo wa madeni ambayo Wizara na Taasisi za Umma zilikuwa zikizalisha kwa kutumia huduma ya malipo ya baada ya ambayo Taasisi nyingi na Wizara zilishindwa kulipa kwa wakati na hivyo kuendelea kuzalisha madeni ambayo yalifanya Wakala kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Serikali kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) imeendelea kuweka mkazo kwa miongozo katika kupata huduma za ufundi na matengenezo zinazotolewa na TEMESA ambapo kwa kipindi cha siku 100 za uongozi wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wakala haujazalisha deni lolote katika utoaji wa huduma za ufundi.

Katika siku 100 za uongozi wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) imeweza kuboresha mifumo ikiwemo mfumo wa E-Mrejesho.

Wananchi wanaopatiwa huduma kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) kwa sasa wanapata mrejesho wa huduma na namna huduma mbalimbali zinavyotolewa na TEMESA kupitia Mitandao ya Kijamii mfano; Instagram, Youtube, Facebook, Twitter X, Thread na TikTok.

Aidha wananchi wanapata fursa ya kutumia simu za bure kuuliza kuhusu huduma za TEMESA mfano huduma za vivuko na karakana na wanaweza kutoa maoni yao kuhusu namna ya kuboresha huduma hizo kupitia mifumo husika. Namba za simu ya bure inayotumika ni 0800110379.

## HITIMISHO

TEMESA inapenda kutoa shukrani zake za dhati kwa Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuiwezesha kusimamia utekelezaji wa majukumu yake katika utoaji wa huduma kwa wananchi. Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan imeonyesha kasi kubwa ya utekelezaji, uwajibikaji na dhamira ya dhati ya kuwatumikia wananchi.

TEMESA pia inaishukuru Serikali kwa kuuruhusu Wakala kuanza kutumia muundo mpya ambao unatoa motisha kwa watumishi wake kuendelea kufanya kazi kwa bidii na kwa weledi mkubwa.



**WAKALA WA UFUNDI NA UMEME TANZANIA (TEMESA).**
TEMESA HOUSE, 2 MTAA WA TEMESA
41104 TAMBUKARELI,
S.L.P 1075, DODOMA.

TELEPHONE: +255 737 962 496
0800 110 379

EMAIL: info @temesa.go.tz
WEBSITE: www.temesa.go.tz

